Wakati gani nitapata chanjo ?

2021

01 Januari :
- Wakazi na watumishi wa vituo vya afya ya makao
- Watumishi wa sekta ya afya (daktari, wauguzi,…) wa hospitali.

02 Februari :
- Watumishi wa sekta ya afya wanao husika na matibabu ya msingi (daktari wa jamaa, wafamasia,…)
- Vituo vya afya ya umma (sekta ya usaidiaji kwa watu wenye ulemavu,…) na watu wanao tumika hospitalini.

03 Machi :
- Watu wa umri ya miaka sitini na tano au zaidi.
- Watu ambao wanakua katika hatari kumbwa kulingana na afya yao.

04 Aprili :
- Watu wanaotumika kazi za muhimu sana

06 Tangu juni :
- Mtu yeyote yule ambaye ana zaidi ya umri wa miaka kumi na nane.

Kalenda hii inaweza badilika. Kwa ratiba ya hivi karibuni, ni heri uchunguze tovuti www.info-coronavirus.be

Nitajua je au namna gani nitajua wakati nitakapo chanjwa ?

- Utapokea aliko kupitia kibarua, ujumbe mfupi na / au pepe. Auna chochote cha kufanya kibinafsi kuusu aliko.
- Unajiorodhesha kupitia teknolojia ya kompyuta au kupitia simu.
- Katika miji zingine, unaweza changua tarehe yako ya kupata chanjo au ya kujichanjisha. Miji zingine zinakutolea pendekezo ya tarehe mbili. Tarehe hizo haziambatane na mpango wako ? Kwa hiyo, unaweza changua tarehe ingine.

Ni wapi ambapo naweza kujichanjisha ?

Katika kituo cha chanjo.

Na chanjo hii ni ya gharama ngapi ? (au chanjo hii inauzishwa ngapi ?)

Chanjo inatolewa bure (bila gharama yoyote)

Kwa taarifa zaidi, fungua ?

www.info-coronavirus.be/
www.laatjevaccineren.be
www.covid.aviq.be/fr/vaccination
www.coronavirus.brussels/vaccination-menu/

V.U.: Regie der Gebouwen / Agence immobilière fédérale / Federaal Vastgoedagentschap / Federale Immobiliënagentschap, Treurenstraat 15, 1000 Brussel / Rue des Tanneurs 15, 1000 Bruxelles / Place Victor Horta 40 | B-1060 Saint-Gille

Swahili

Wende jichanjisha !

Francophones Bruxelles · brussel · Iriscare · COMMISSION COMMUNAUTAIRE COMMUNE · GEMEENSCHAPPELIJKE GEMEENSCHAPSCOMMISSIE · .be

Namna gani chanjo zinatumika ?

- Kupitia chanjo, mwili wako unatengeneza kingamwili.
- Vitu hizi zinasaidia kwa kupinganisha chembe cha virusi.
- Unawasiliana na janga la virusi ya corona baada ya hapo ? Kingamwili hizi zitakulinda.

Kwa nini chanjo inashauriwa ?

- Virusi ya corona inaweza onekana kuwa hatari sana kwako binafsi na kwa watu wengi wanaokua karibu nawe :
  - ✔ Watu wa umri ya miaka sitini na tano na zaidi.
  - ✔ Watu wanaouguwa magonjwa ya mapafu, ya moyo au ya mishipa.
  - ✔ Watu wanaougua magonjwa ya kisukari au shinikizo la damu.

  Lakini virusi inaweza pia kua hatari kwa watu ambao ni vijana na wenye afya bora.
- Ikiwa asili mia sabini ya watu (70%) Ubeljiji wanapata chanjo, kusambaa kwa virusi kutapunguka. Ni hiyo inaitwa « kinga ya kundi »
- Maisha yako itarejesha haraka zaidi hali yake ya kawaida.
- Mwili wako utajilinda vizuri zaidi dhidi ya virusi.

Chanjo itatumikishwa namna gani ?

- Kuna aina mbalimbali za chanjo.
- Kwa aina fulani ya chanjo, sindano moja inatolewa juu ya mkono wako. Baada ya sindano, unapashwa chunga siku kumi na tano kwa kiwango cha chini. Kiisha, chanjo litakukinga iwezekanavyo dhidi ya virusi ya corona.
- Kulingana na hali ya chanjo ingine, sindano inatolewa kwanza na baada ya wiki fulani, sindano ya pili. Baada ya sindano ya pili, unaweza pia chunga siku kumi na tano kwa kiwango cha chini kwa kupata kinga bora kabisa.

Chanjo ni yenye uhakika ?

- Kunakua utaalamu mkubwa zaidi kuhusu utengenezaji ya chanjo. Wanasayansi na wataalamu wakifamasia wa dunia nzima waliendeleza chanjo katika muda mfupi. Kulikua pia pesa ya kutosha na muda kwa kufanya kazi hiyo kwa sababu ilikua jambo la haraka. Wakati huo huo, watu wengi wamekwisha tayari kujichanjisha (au tayari wamekwisha kupokea chanjo yao).
- Chanjo imechunguzwa kabisa na wanasayansi wenye mamlaka. Kweli, ni chanjo yenye uhakika.

Ni katika hali gani sipashwi kuchanjwa ?

Kwa kawaida, mtu mzima wowote anaweza chanjwa. Unaweza pia kujichanjisha ikiwa uko mjamzito, au ikiwa unanyonyesha. Una maswali kuhusu jambo hilo ? Ni heri kuziuliza daktari wa familia yako mbeleni.

Kuna jambo fulani za pekee :

- Umewai kupata mzio ya haraka au ya nguvu zaidi baada ya chanjo ya hapo mbele ? Au ulipata haja ya matunzo za ki afya kiisha kutumia dawa ? Ikiwa ni hivyo, ni heri zaidi uwasiliane na daktari wa familia yako mbele ya yote.
- Unakua na alama ya ugonjwa wa kuambukiza (sawa vile homa ya zaidi ya digrii thelathini na nane (38°)). Kwa hiyo, usichukue mpango fulani kuhusu chanjo kabla ya kupona kabisa.
- Umefanya kipimo ya kufuatilia iliyoonyesha kama unaugua virusi ya corona na aukugonjwa mnamo siku kumi na tano zakufuata ? Unaweza chukua mpango.
- Umefanya kipimo ya kufuatilia iliyoonyesha kama unaugua virusi ya corona na unagonjwa (au un-augua virusi ya corona) : Wasiliana na daktari wa familia yako. Aupashwe kuchanjwa kabla ya siku kumi na tano baada ya kupona kwako.

Je naweza sikia athari (au vinyume) baada ya chanjo ?

Inawezekana usikie athari (vinyume) zifuatazo :

- Kubadilika kidogo kwa mwili kua nyekundu, maumivu au mwili kuvimba kidogo juu ya mkono (pale ulipata chanjo)
- Mchoko
- Maumivu kichwani
- Ongezeko isiyo kumbwa (au ongezeko ndogo) ya temprecha

Ni kawaida na aiko ya kutisha. Unaweza tumia paracetamol. Sawa mtu mzima, tumia kidonge moja au vidonge viwili (500 mg hadi 1000 mg) baada ya saa inne au sita kila mara kufuatana na haja yako. Unaweza chukua gramu tatu kwa siku kwa kiwango cha juu.
Una mashaka au malalamiko yanayoendelea ? Ikiwa ni
hivyo, ni heri zaidi
kuwasiliana na daktari wa familia yako.

Lakini uendelee kuheshimu maelekezo hadi watu wakutosha watapata chanjo. Heshimu umbali wa mita moja na nusu kati yako na wengine, vaa barakoa ao mask yako na osha mara kwa mara mikono yako.